

**UFALME WA MUNGU KWA WATU WOTE!**  
**Dr. Martin Jäggle/ Sr. Teresa Schlackl SDS**  
**12 Julai, 2015**

“Ndio, Tusali kwa bidii sana na tufanye kazi ili lengo la Yesu ‘ufalme wako ufike’,  
lipate kutimizwa.”<sup>1</sup>

Somo la Kumbukumbu ya Kiroho linaonyesha: Baba Jordani alielewa kwamba watu wote wanaume na wanawake wapo katika Ufalme wa Mungu. Jordani aliwataka watu wote wavutiwe na Ufalme wa Mungu. Kadri yake “Utawala wa Mungu” ulikuwa umesambaa, ulikuwa wa ulimwengu, ulikuwa kumbakumba, ‘makao’ pekee yasiyoweza kupotezwa.

**1. Ufalme wa Mungu na Haki yake katika Ulimwengu: Mtazamo mwingine wa Maisha**

Nia kubwa ya Baba Jordani ilikuwa ni “kujitoa kwa Mungu na Ufalme wake” ambao alikuwa ameuelewa kama “ufalme wa mapendo.” Ufalme wa Mungu na haki yake ni “kitu kama moto uwakao ndani na mwanga, ambao unaonyesha njia kuelekea ufuasi wa Yesu, ambao unanisaidia kutekeleza mtazamo wa kweli, salama na kupata uzima kwa watu wote, hapa katika dunia hii na kabla ya kifo.” Ufalme wako ufike” tunasali – kama inavyofundishwa kwenye desturi za Kiyahudi – siku kwa siku. Kwa hilo, tamaa ipo wazi. Sauti ya kilio – kama tunavyojua kutoka kwa Batimayo – ni kwa ajili ya maisha salama. Ni tamaa ya ujio wa Ufalme wa Mungu.

**“Ndio, tusali kwa moyo na  
kufanya kazi mpaka  
mapenzi ya Yesu, ‘ufalme  
wako ufike’, yatimizwe.”  
Mwenyeheri Maria wa  
Mitume: Barua, Mei, 20,  
1901**

Kiini cha matamko ya Yesu – ujumbe kwamba Ufalme wa Mungu umeanza tayari na upo (Mk 1, 15) – umeunganishwa na haki/ unyoofu. Mabadiliko ya moyo ni ya muhimu pia kama njia ya kuondoa udhoofishaji wa miundo, ambayo matokeo yake yanasababisha uonezi na utengano.

*Sheria ya Familia ya  
Wasalvatoriani Sura ya 3  
Utangulizi*

**Ufalme na Changamoto Yake**

“Kwa kusoma Maandiko Matakatifu inaonyesha wazi kwamba Injili haihusiani tu na uhusiano wetu binafsi na Mungu. Wala majibu yetu ya upendo kwa Mungu yasionekane kama mkusanyiko wa ishara ndogondogo binafsi za watu walio na mahitaji, aina ya upendo maalum, au mlolongo wa matendo unaolenga hasa kutuliza dhamiri zetu. Injili inahusu Ufalme wa Mungu (LK 4.43); Inahusiana na Mungu mwenye upendo ambaye anatawala ulimwengu wetu. Kwa kadri ambavyo anatawala ndani yetu, maisha ya jamii yanakuwa ni mfumo wa undugu, haki, amani na utu duniani.” (EG 180)

Sehemu ya Ufalme wa Mungu ni mahusiano halisi ya wanadamu na jamii; wale ambao wapo kwa namna ya pekee katika “nchi” ya Mungu, ambapo anaishi. Kwa hiyo Jumuiya (qahal/ekkleisia) za Wayahudi na Wakristo zinaweza kuangaliwa kama ‘sehemu za uzoefu’ na ‘ndoto halisi za Ufalme wa Mungu, kama kuanza kwa ufalme wa Mungu.

---

<sup>1</sup> Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani III, Maria wa Mitume: Barua, Mei 20, 1901.

## **Ufalme wa Mungu Kama Sikukuu ya Wazi “ya Mlo wa Pamoja”**

Nyanja za uchumi, siasa, utamaduni na dini ni sehemu ya sherehe moja.

- Ya kutosha ni sehemu ya sikukuu hata kama kuna mida mingine maisha ni ya huzuni.
- Kufanyasi kukuu ni muhimu, yaani kila mmoja ana sehemu yake na hakuna anayebaguliwa.
- Wakati wa sikukuu mtazamo kwa maisha mema kwa kila mmoja unaonekana.

“Meza ya duara” ya mlo wa Sikukuu ni njozi ya jamii, ambayo ipo wazi kwa kila mtu. Sikukuu huwapa wote uzima tele – chakula, jumuiya na maana.

Kwa Yesu Ufalme wa Mungu ni jamii isiyo na maskini, jamii iliyo tayari kuwa na mshikamano na haki, na ambayo inajali zaidi mahitaji ya watu.

Ufalme wa Mungu unaelezwa na Yesu kama chakula kwa wale wasiokosa kitu katika jamii. Watu wazima wanawajali watoto. Wanawake wana utu, wanaheshimiwa na kazi zao zinaonyeshwa kwa watu (Mt. 13, 33). Ni ufalme wa undugu usio wa mabavu.

Upatikanaji wa ufalme wa Mungu unatolewa kwa desturi fulani (Mt 7, 21). Kwa Yesu Ufalme wa Mungu una maana kwamba mashetani ambao wapo dhidi ya Mungu na Uzima hawana nguvu tena.

Papa Fransis alisema wazi kwamba ana mahitaji, ya Waamini na sala zao. Ufalme wa Mungu ni wenye usawa, mkusanyiko ulio wazi wa watu wenye mahitaji, ambao wameshikamana na ambao wanafahamiana kama watu walio sawa na fukara.

Kama ufalme wa Maskini, Ufalme wa Mungu ni dira ya jamii ambapo hakuna anayeteseka na njaa na kila mmoja anapata “kilicho muhimu kwa usala wa kiuchumi na utimilifu wa uzima wa Utu.” Ni mtazamo wa ulimwengu mmoja ambapo kuna “vitu vya kutosha kwa ajili ya wote.”

Kama Ufalme wa “Jamii isiyo na mwenyewe” Ufalme wa Mungu ni dira ya jamii ambayo hakuna hata mmoja anayedharauliwa, anayenyanyaswa au kutengwa. Kama Ufalme “ambao mapenzi ya Baba yatatimizwa, ufalme wa Mungu ni mtazamo wa jamii – ambapo hakuna hata mmoja anayesumbuliwa na pepo, ni ufalme ambapo sheria yake ya msingi ya mapenzi ya Mungu na mapendo yapo dhahiri.”

## **2. Uwepo kama Nafasi ya Ufahamu wa Ufalme wa Mungu**

Kwa Israeli “wokovu wa kidini hauwezekani bila kuwa na haki katika mji wa dunia. Yerusalemu ya duniani inahitaji kukamilishwa (...) ili kwamba Yerusalemu ya mbinguni iwe imejazwa na uwepo wa Kimungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu, zaidi ya ile ambayo watu wanaishi.” Ufalme wa Mbinguni ni zawadi na pia ni wajibu. Utawala wa Mungu ni ahadi kwa wakati ujao, ambao kutokana na mtazamo wa Agano la Kale linatimilika kwa kupitia uhamisho.

Yesu wa Nazareti aliishi katika desturi hii. Katika kiini cha maisha yake ni ujumbe wa Ufalme huu wa Mungu: “Wakati umewadia na Ufalme wa Mungu umekaribia, tubuni na kuiamini Injili.” (Mk 1, 15) Hakuna mada iliyomsumbua Yesu mno kuliko ‘basileia tou theou’,<sup>2</sup> mawaidha ya

---

<sup>2</sup> Maana yake ni: “Ufalme wa Mungu” ambao una maanisha uhalisia wa kiroho na ufalme wa Mungu, nguvu ya kifalme na utu.

utawala au ufalme wa Mungu.” Ukweli kwamba Yesu, mwenyewe, alifahamu kwamba “kutoweza kutulia” kama vile Muhubiri anayezunguka kwa miguu, inatuonyesha pia jinsi dhana hii ya uhamaji ilivyo muhimu kwa utambulisho wa Ukiristo.

Kutokana na ukweli kwamba Mungu kutoka mwanzo kama Muumba ni mfalme wa Ulimwengu, ambaye ameshafahamika na watu wa Agano la Kale – pia na Yesu. Hata pamoja na Yesu Mungu haji karibu nasi kama zamani: kipindi cha ukombozi kutoka Misri “Kidole cha Mungu” (Kut. 8, 15) kilikuwa kinatenda kazi kama ilivyokuwa katika kipindi cha kufukuza mapepo wakati wa Yesu (LK 11, 20). Yesu kila wakati alihusisha kazi yake na kazi ya Mungu. Yesu anaelewa Ufalme wa Mungu katika desturi zake za imani ya Kiyahudi. Ambacho kilikuwa ni kipya na uhakika usiyoyumbishwa na ahadi ya uwepo wa Mungu. Kwa nyongeza kitu kilicho kipya ni sheria fulani za desturi za Kiyahudi. Mabadiliko endelevu ya maana ya nguvu na mamlaka katika huduma ya uzima ikihusisha kukosa uzima juu ya msalaba kama nguvu ya kuokoa.

Kupitia Yesu wa Nazareti utawala wa Mungu unakuwa ni ufunguo wa elimu na kiini cha mafundisho yake. Yaani ni kitu kipya ambacho anakitengeneza katika maisha ya kila siku ya watu walio wanyofu na walio maskini. Uwepo wa Mungu usiogawanyika ni kiini cha matangazo na desturi ya Yesu wa Nazareti: kwa sasa ufalme wa Mungu upo tele; na sasa ahadi za kinabii zimetetelezwa. Uwepo huu unaweza ukabadilishwa ukawa uzoefu wa ufalme wa Mungu. Uwepo huu unakuwa ni saa ambayo wokovu wa Mungu unakamilishwa. Ufalme wa Mungu unapatikana kwa ajili ya watu (Lk. 17, 20). Upo dhahiri ulimwenguni: “katikati yenu.” Matokeo ya kufuru kwa “kanisa” yanaonekana; utawala wa Mungu unafanyika katika maisha ya kila siku. Unakuwa ni kitu halisi katika matendo ya ulimwengu kama vile usimamizi wa fedha, mshahara, madeni, n.k.

Kutoka enzi za Yesu wa Nazareti, sasa ufalme wa Mungu upo tele. Utawala wa Mungu unafanyika katika maisha ya kila siku na katika matendo ya kidunia.

## **Kuishi Pamoja**

Ufalme wa Mungu ni mtazamo wa kuishi kwa pamoja. Hitaji kwa ajili ya haki ni muhimu na linahusiana na swali kwamba namna gani tunahusika na swala la uhamiaji. Wazalendo wangeweza kukumbuka mtazamo huu kwa sababu waliwaona wahamiaji kama watu waliokuwa wakitangaza Ufalme wa Mungu. Kwa kuishi pamoja kungekuza mahali ambapo Ufalme wa Mungu ungekuwa ni uhalisia. Kukua kiroho kunahitajika kama ni uwezekano kwa ajili ya uzima ambao Mungu mwenyewe aliahidi. Hapa mfano wa Theo Sundermeir ni msaada: kuishi pamoja, kujifunza kutoka kwa kila mmoja, na kusherekea pamoja.

## **“Jumuiya ya Haki”**

Njia ya kawaida ya Muumini ni ya “jumuiya ya haki,” ambayo waliishi kutoka ufahamu wa Ufalme wa Mungu na haki yake. Kwa hiyo haki haihitajiki kufanywa, bali inahitaji kuonyeshwa. Desturi ya haki “inapatikana katika kuutafakari ujuzi wa Mungu, ambao tunautarajia utoke kwa Waamini ambao ni tofauti na pia ni haki ya juu ambayo inasimama katika upeo wa fikra ‘kama ilivyotolewa bure.’”

## **Yaliyomo katika Maisha ya Kiroho na Fumbo la Ufalme wa Mungu**

**Maana ya Uhalisia** “Maisha ya Kiroho yanamaanisha roho ‘ambayo katika hilo mtu anakabiliana na uhalisia.’ “Uhalisia ni mkubwa zaidi kuliko fikra. Kanuni hii inahusiana na umwilisho wa Neno

na kuwekwa katika matendo (...) Kufanya kazi za haki na mapendo ambayo inafanya neno hilo kuzaa matunda.” (EG 233)

Kutokana na Jon Sobrino<sup>3</sup> Maisha ya Kiroho yanategemea “1. Unyoofu wa msingi ili kuona uhalisia kama ulivyo; 2. Uaminifu wa juu kwa uhakika huo; 3. Utayari wa kuhusisha ya “zaidi ambayo yana uhalisia huo na unabebwa nao.”

Maisha ya kiroho ya kipekee yanahusiana na maisha halisi; siyo ya ubinafsi, na hii ina maana ya ufuasi. Kama maisha ya Kiroho ya uzima hii inatusaidia kutumika kama mtazamo wa maisha yaliyo kamili na yenye utu kwa watu wote.

- “Zawadi ya Mungu kama wajibu wa lazima”
- “Upo lakini bado haujakamilika”
- “Katika Ulimwengu na kwa ajili ya ulimwengu lakini usio wa Ulimwengu”
- Alama ya uwepo na ushuhuda wa matendo

### **3. Majitoleo – Tutaidumisha Vipi? (Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani)**

Naomba mniruhusu tena kumnukuu, Papa Fransis ambaye aliongozwa na Maandiko Matakatifu: “Mungu kila wakati anaendelea kuwafanya upya watu wake, bila kujali umri wao: ‘wataruka juu kwa mabawa yao kama tai, watakimbia na hawatachoka, watatembea na hawatakuwa dhaifu.’” (Isa 40:31) (EG 11).

Kwa hiyo tunaweza kushughulikia swali hili: ni namna gani tunaweza kuweka hai ahadi tukiwa katika hali fulani ya utulivu? Nimevutiwa sana na “sheria ya Familia ya Wasalvatoriani.” Ni hati inayoongea kuhusu majitoleo ya dhati kwa ajili ya utangazaji wa Injili ya Yesu Kristo, ambayo inatoka kutoka ufahamu mkuu wa Mungu. Kwa njia mbalimbali Sheria hii inaendana na wakati tulio nao.” Ni hati ambayo inaongea kwa uhakika kama Baba Jordani na Mama Maria wa Mitume. Sheria hii inawaalika wengine wajiunge na Familia ya Kisalvatoriani.

Kama nikiangalia Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani na nikijikita katika “Maisha ya Kiroho ya Ufalme wa Mungu,” tunaweza kupata huko taarifa mbalimbali zinazolingana. Wewe mwenyewe **utajua** jambo hili. Kilichonivutia sana ni msisitizo juu ya “ushirikiano na watu wenye mapenzi mema.”

Swali letu hapa ni<sup>4</sup> “majitoleo” – tutawezaje kuyaweka hai? Katika kujibu swali hili nilialikwa kutoa vipengele vichache. Kitu gani ambacho kinaniwezesha kufanya hili isipokuwa ukweli kwamba nilikaribishwa kuongea hapa, ambayo ina maana kufikiria kwa sauti? Tafadhali msitarajie kupata jibu la mwisho, suluhisho. Amua wewe mwenyewe kama mawazo yangu yanastahili kupewa uzito kwa ajili yako.

---

<sup>3</sup> Jon Sobrino: Der Geist, der befreit. Anstosse zu einer neuen Spiritualität, Freiburg i. Br. 1989, 27. (Ni roho ambayo inakomboa. Mtazamo wa Maisha ya Kiroho ya Sasa).

<sup>4</sup> Martin Jaggie alikuwa ni mtoa maada katika Mkutano wa Kamati ya Kimataifa ya Muungano wa Karama (IJCC) mwaka 2014.

## **Nadhani ni muhimu kukumbuka mambo matatu:**

1. Kiwango ambacho mawazo ya msingi ya sheria ya Familia ya Kisalvatoriani ambayo tunaweza kuyaishi; inategemea na kiwango cha ushiriki wakati hati ilipokuwa ikiandikwa. Inawezekana vipi wale watu ambao wanaishi mawazo haya ya msingi wanayafanya kuwa maisha yao?
2. Motisha ni swala mtu binafsi lakini si swala lake mwenyewe. Yeyote aliye na wajibu katika taasisi au jumuiya hawajibiki kutoa motisha kwa kila mwanachama binafsi, bali katika mazingira yanayowasaidia wananchama kutunza motisha zao.
3. Unaweza kuona umuhimu wa mawazo ya msingi katika jumuiya au taasisi katika ‘kuyawezesha’. Hii ina maana miundo, mifumo, mila, njia ambazo zimerasimishwa katika taasisi ambazo fikra hizi “zinatekelezeka”. Tunaongea juu ya kumwilishwa kwa Roho. Ni miundo, mifumo n.k. gani iliyopo au ina uwezekano, katika roho gani ya jumuiya inapo “fanyika” kama ilivyoonyeshwa katika wazo la msingi?

Je, lugha na mawazo ya sheria ya Familia ya Kisalvatoriani yanapata uhalisia wa “zaidi”, “muundo wa neema katika uhalisia”?

## **Matokeo ya Usalama**

Kwa ajili ya maisha ya kiutu na bila ya uwoga, kiasi fulani cha usalama wa kiuchumi ni muhimu kwa uhakika wa namna ya kuishi. Usalama unaboresha maendeleo ya umuhimu wa mtu. Lakini niliona matokeo ya idadi kubwa ya mikataba ya makarani, ambao walipunguza majitoleo yao ya kiutu na walifanya kazi kwa muda mrefu bila furaha. Ni yule tu aliyekuwa na ujuzi wa kuweza kutambulika anaweza kufikia fursa za hali ya juu.

## **Kupata Chanzo**

Kuwa “moto na kuwaka”, “kuchomwa” kwa kitu au mtu ni vielelezo ambavyo vinaonyesha mtu ambaye “amechochewa”, mtu ambaye ni hai “mwenye furaha tele.” Kila ishara ina maana zinazohitilafiana. Moto pia unaweza kuchoma, kuteketeza au hata kuharibu. Kwa hiyo msemu kwamba “ungua” ni maelezo sahihi ya ugonjwa wa muda. Kwa hiyo Napata kigugumizi kusema kwamba “moto na mwanga” isipokuwa katika hali fulani ambapo “moto uliotulia” au “moto mdogo” ni muhimu. Na kama isingekuwa hivyo, pale tu moto unapopungua, ujasiri wa kuweza kustahimili – licha ya yote – ingewezekana kuonekana? Kwa hali yoyote ile, shauku haiwezi kuamshwa au kupatwa.

Lakini kinachoweza kupatikana ni njia ya kufikia chanzo ambacho kutoka hicho jumuiya na wanachama wake wanaishi. Hapa inawezekana kielelezo cha maji ya ardhini ni msaada, kama chanzo njia ya kufikia chanzo kikipotea – kwa sababu yoyote ile – uhai na uzima vitapotea. Watu hao wamenyauka, wamekuwa wagumu, kama wafu.

Wewe mwenyewe unafahamu vizuri sana nini na wapi vilipo vyanzo hivi na mnaweza kuvipataje na kuendelea kuvifikia. Kama watu tunategemea vyanzo vya maji, lakini kwa wakati huohuo hatuwezi “kutengeneza” maji/chemchem. Shughuli yetu ni kunywa tu. Yeyote anayekunywa kutoka chanzo ataburudishwa, ataimarishwa na atakuwa hai. Hii itaimarisha ujuzi wa kujifahamu na fursa za mtu zitatolewa kama zawadi. Ufahamu huu unaimarisha shukrani. Mwendelezo wa kuwa na shukrani unakuza tamaa ya kufikia ujuzi wa wengine.

Ningependa kukumbusha hapa upande mmoja wa “maisha ya kiroho ya Ufalme wa Mungu”, ambayo niliyaeleza hapo awali: kama zawadi nzuri, ufalme wa Mungu ni chanzo cha shukrani. Pamoja na ufalme huu mtazamo ulishuhudiwa na Yesu wa ukweli, aliponya na una uzima ulio kamili unaoahidiwa kwa watu na unatoa maana kwa ajili ya uzima wa kila mmoja. Hii inampa mtu uhuru wa kuamini katika maisha haya licha ya yote ambayo yanawazuia kuachana na uzima au kuishi kwa ndoto ya kuweza kupata” kila kitu.” Je, lengo haliwezi kutoka kwenye shauku na kuchukua mwelekeo wa shukrani?

## Umuhimu wa Uhalisia

Kuhusiana na “majitoleo – tutawezaje kuudumisha?” Niliogundua vipingamizi vinavyotarajiwa:

- a) Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani inaongelea juu ya watu **wote**. Bila shaka swala hili linaweza kumaanisha kwamba hakuna mtu yeyote anayebaguliwa. Laini hayo sio matokeo yanayoonekana kuwafikia wote: Je, tunataka kuwafikia watu wote au ni lazima kufika kwa watu wote? Na tunapimaje “mafanikio”? kama mtu mmojammoja ameitwa na Mungu katika hali ya upekee, hivyohivyo watu hao hao wanatumwa kwa watu maalumu katika hali za upekee. Amri ya Utume “Nendeni na myafanye mataifa yote kuwa wafuasi wangu” inatumika kwa Kanisa zima, na sio kwa mtu mmojammoja au jumuiya ambayo inashiriki amri hii ya utume.

Swali ambalo linazuka ni hili: Hawa **wote** ni nani? Sheria inasema **wote**, lakini tunamaanisha wote kwa uhalisia wake?

- b) Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani inaonyesha mfano ambao watu wanatakiwa kuvutwa na kuwa changamoto. Lakini hakuna uwezekano wa kufanya hivyo, kwa kufanya majaribio, kwa kutafuta fursa, bila kuangalia nyuma, bila udhaifu, bila kuanguka, bila kushindwa, bila kujitegemea, bila kuwa na hitaji, na wala bila kufanya kwa sehemu. Matokeo yake yatakuwa ni kuwa na msimamo, kutokwazwa na wala kutojisikia faraja kwa ajili ya wanajumuiya wote. Vipingamizi, au nafasi za giza, ya kuwa mwanadamu na Mkristo havirekodiwi. Lakini, unapokuwa katika desturi ya mambo hayo yote, uhalisia hauwezi ukaja hata siku moja.
- c) Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani inajali sana kuendana na alama za nyakati na watu wote wenye mapenzi mema. Labda ufalme wa Mungu upo hapa na unajumlishwa katika alama za nyakati ambazo hazionekani. Leonardo Boff aliliongelea jambo hili kwa namna hii Mungu anafika kabla ya Wamisionari kufika. Lengo la kuonekana kwa matendo ya kutoka kwa Mungu kwa sasa yanawasaidia watu – kupitia vilio vyao kwa ajili ya ukombozi – wagundue kwamba uhalisia wa “zaidi”, matumaini na ahadi zake.

Mwanzoni, nilionyesha kwamba swali muhimu juu ya maisha ya Kiroho ni “swala la uhusiano kati ya maisha ya kiroho na uhalisia.” “Maisha ya kiroho yana maana ya kwamba roho ambayo mtu anaweza kukabiliana na uhalisia.” Jambo hili lilimwongoza Papa Fransisi:

“Uhalisia ni muhimu sana kuliko fikra (...) uhalisia ni mkubwa sana kuliko fikra. Hii inatutaka kukataa njia mbalimbali za kuigiza uhalisia: mtindo wa utakatifu wa kimalaika, udkiteta wa kutojali (relativism), ufasaha wa lugha usio na maana, malengo ya kufikirika zaidi kuliko uhalisia, alama za kihistoria zisizobadilika, mifumo ya maadili isiyo na wema, mazungumzo ya kitaalamu yasiyo na hekima (EG 231)

Uhalisia una wingi wa wasiwasi na mabishano; uhalisia hauingizwi kaika sheria na taratibu. Maswali yanayokuja ni: lugha na matarajio ya sheria yameathiri kiasi gani kuzuia au kuharibu njia inayotuelekeza kwenye uhalisia? Je, lugha na matarajio yanatusaidia kupata huu uhalisia wa ‘juu’, “muundo wa neema katika uhalisia”? Yoyote atakayeona muundo huu wa neema atatoa jibu kwa roho ya shukrani na katika utambuzi wa kuwa amepata zawadi. Kwa hiyo “utayari wa kukua katika uhusiano kuelekea uhalisia upo katika ‘ziada na unabebwa nao.’”

Inawezekana njia hii kuelekea uhalisia inatuonyesha uhusiano kwa jumuiya na watu binafsi “kuweka majitoleo yao hai.”

Kwa hitimishi, ninakazia tena kipengele cha maisha ya kiroho ya ufalme wa Mungu, ambao unasema kwamba Ufalme huu upo sasa lakini bado haujakamilishwa vya kutosha.

Maisha ya kiroho ambayo yanatuelekeza katika ufalme wa Mungu ambao unaamini kwamba yote yana maana na yatadumu mbele ya Mungu, kwamba yote yatafanyika kwa jina la Ufalme wa Mungu, hata kama upo katika hatua ya mwanzo na isiyokamili. Maisha haya ya kiroho yanatutia moyo kuamini katika umaana ambao tupo nao sasa – katika namna ya ufalme wa Mungu – ambao unaweza kuonekana na kushuhudiwa kama ‘uzima wa milele’

### **Maswali ya Tafakari**

1. Soma tena Sheria za Familia ya Kisalvatoriani kwa mwanga wa makala hii.
  - a. Onyesha maneno au misemo ambayo inakugusa na ujiulize, “jambo hili linaniambia nini mimi na nitalipa mwikio gani?”
  - b. Manufaa yake yanaweza kuwa ni yapi katika familia ya Kisalvatoriani katika eneo lako la ulimwengu au/na kwa ulimwengu mzima?
2. Kwa mwanga wa makala hii, kama ukiamua kuitengeneza upya sheria ya familia ya Wasalvatoriani, Je, Utaongeza kitu gani au kukibadili?
3. Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani inaongea juu ya “watu wote” hawa “wote” ni kina nani? Sheria ya Familia ya Kisalvatoriani inasema wote, lakini kwa uhalisia tuna maana ya wote?
4. “Maisha ya Kiroho ina maana ya roho ambayo mtu anaitumia kuweza kukabiliana na uhalisia.” Papa Fransisi anasema “uhalisia ni mkubwa kuliko fikra” (Evangelium Gaudium 231). Hii inatuelekeza katika swali la uhusiano uliopo kati ya maisha ya kiroho na uhalisia. Ni kwa njia gani maisha ya kiroho ya Wasalvatoriani yanajitokeza tena katika uhalisia wangu?